# Nafasi ya Kiswahili katika Sanaa, Michezo na Utamaduni kwa Nchi na Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

*Ahmad Y. Sovu*

## IKISIRI

*Makala hii inachunguza nafasi ya Kiswahili katika sanaa, michezo na utamaduni katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikilenga kubainisha mchango wake katika kuimarisha mshikamano, utambulisho na ubunifu. Utafiti umejikita katika Nadharia ya Uchanganuzi Tunduizi Kilongo ya Norman Fairclough (1995) na kuungwa mkono na Nadharia ya Itikadi za Lugha ya Woolard (1998), ili kufafanua matumizi ya lugha katika muktadha wa kijamii na athari za mitazamo kuhusu lugha hiyo. Data zilikusanywa kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda kupitia usaili na hojaji za mtandaoni, zikihusisha watoataarifa 30 ambapo kila nchi waliteuliwa 6, wakiwamo wahadhiri wa Kiswahili, wasanii, wanamichezo, wanahabari na wataalamu wa lugha. Uchambuzi wa data ulifanywa kwa mkabala wa kimaelezo kwa kuainisha mada kuu na vielelezo halisi vya kauli za washiriki. Matokeo yanaonesha kuwa Tanzania na Kenya zinaongoza katika matumizi ya Kiswahili kwenye sekta husika, ilhali Uganda, Burundi na Rwanda ziko katika viwango vya kati na vya chini. Kiswahili kimethibitishwa kuwa nyenzo muhimu ya mawasiliano ya kisanaa, mshikamano wa michezo na utambulisho wa kikanda. Changamoto zilizobainika ni pamoja na mitazamo hasi, udhaifu wa sera za lugha na uhaba wa wataalamu. Makala inapendekeza kuimarishwa kwa sera za lugha, ufundishaji wa Kiswahili na uwekezaji katika sekta husika kwa maendeleo jumuishi ya JAM.*

# 1.0 Utangulizi

Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM) ni shirikisho la kikanda linalojumuisha Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Somalia. Ilianzishwa rasmi mwaka 2000 kufuatia kusainiwa kwa Mkataba wa JAM, baada ya kuvunjika kwa jumuiya ya awali mwaka 1977. Lengo lake ni kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa maendeleo ya pamoja (EAKC, 2019). Hivyo, Kiswahili kimetambuliwa kama lugha ya mawasiliano na chombo cha kujenga utambulisho na mshikamano wa kikanda. Kiswahili ni lugha ya Kibantu iliyokua katika mwambao wa Afrika Mashariki kupitia biashara, dini na mwingiliano wa kihistoria. Kilienea bara na baadaye kuimarishwa wakati wa utawala wa kikoloni na baada ya uhuru, hasa kupitia sera za lugha za Tanzania zilizoipa hadhi ya taifa (Kiango, 2015). Kwa sasa, zaidi ya watu milioni 200 wanakitumia na kimetambuliwa na taasisi za kikanda na kimataifa kama lugha ya mshikamano na mawasiliano mapana barani Afrika. Hadhi hii imekifanya kuwa nyenzo muhimu ya mawasiliano ndani ya JAM.

Katika sanaa, michezo na utamaduni, Kiswahili kina nafasi ya kimkakati, yaani ya kuweka mipango kwa ajili ya maendeleo. Muziki, mashairi, maigizo na filamu hutumia Kiswahili kufikisha ujumbe kwa hadhira pana ya kikanda. Katika michezo, lugha hii huunganisha wanamichezo na mashabiki na hutumika katika mashindano ya kikanda kama chombo cha mawasiliano na utambulisho (EAKC, 2019). Vilevile, katika hafla za kijamii na matamasha ya kikanda, Kiswahili hutoa jukwaa la pamoja la kuwasilisha mila na desturi. Matumizi haya yamechangia kukuza tasnia ya ubunifu, ajira na diplomasia ya kitamaduni.

Hata hivyo, changamoto bado zipo, baadhi ya nchi za JAM hazijatekeleza kikamilifu sera ya lugha wala kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili katika mifumo ya elimu. Aidha, ushawishi wa Kiingereza na Kifaransa katika sekta rasmi unaendelea kuwa mkubwa. Licha ya hayo, juhudi za taasisi za kikanda kama Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki zinaendelea kuimarisha hadhi ya lugha hii. Makala hii, kwa msingi huo, inachambua nafasi ya Kiswahili katika sanaa, michezo na utamaduni ndani ya JAM kwa lengo la kuibua fursa, changamoto na mwelekeo wa kisera unaoweza kuimarisha mshikamano wa kikanda.

## 1.1 Muktadha wa Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kiswahili kilipata hadhi ya kuwa moja ya lugha rasmi za JAM kupitia marekebisho ya Mkataba wa JAM mwaka 2017. Baraza la Wakuu wa Nchi lilipitisha azimio la kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi sambamba na Kiingereza. Uamuzi huu ulitambua nafasi yake ya kihistoria kama lugha ya mawasiliano ya pamoja katika Afrika Mashariki (EAKC, 2019). Kwa muda mrefu, Kiswahili kimekuwa kiungo cha kijamii na kiutama duni katika ukanda huu. Tangu kutambuliwa rasmi, kimetumika katika nyaraka za jumuiya, mikutano, hotuba na tafsiri za sheria. Hatua hii imeongeza uwazi wa kiutawala na kuimarisha ushirikiano wa kikanda.

Pamoja na hali hiyo, maendeleo na matumizi ya Kiswahili katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, yamekuwa yakitofautiana kutokana na hulka ya kila nchi kuchukua hatua zake bila kushirikisha nchi nyingine hali ambayo imesababisha kukosekana kwa juhudi za pamoja katika kukabiliana na changamoto za ukuaji wa matumizi ya Kiswahili. Kwa mfano, nchini Tanzania, Kiswahili ni lugha ya Taifa, lugha rasmi katika shughuli za serikali na bunge, lugha inayotumika kufundisha shule za msingi na kama somo katika elimu ya juu. Kiswahili kinatumika kutoa mafundisho ya dini, makanisani na misikitini. Kiswahili ni lugha kuu inayotumika katika vyombo vya habari kama vile televisheni, redio na katika idadi kubwa ya magazeti ikiwamo mitandao ya kijamii.

Kwa upande wa Kenya, Kiswahili ni lugha ya Taifa. Katiba ya Kenya ya mwaka 2010, Ibara ya 7(i), imekipa Kiswahili sura mpya ya kuwa lugha rasmi na lugha ya taifa. Aidha, Kiswahili hufundishwa na kutahiniwa shuleni na vyuoni. Fauka ya hayo, lugha hii inatumika bungeni na katika kuendesha biashara. Kiswahili ni lugha kuu ya mawasiliano wanapokutana watu wa makabila tofautitofauti. Kiswahili kinatumika katika jeshi na polisi. Ni lugha ya kuendesha kampeni za kisiasa mijini na vijijini. Vilevile, Kiswahili kinatumika katika kuendesha ibada misikitini na makanisani. Pia, vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili nchini Kenya bado ni vingi, Kiswahili kinatumika katika programu kadhaa redioni na kwenye televisheni. Aidha, Kiswahili kinatumiwa sana katika mawasiliano ya mitandao ya kijamii na blogu za watu binafsi.

Nchini Uganda, Kiswahili kimeanza kutumika kwa mapana na marefu kutoka 2005. Kiswahili kinafundishwa na kutahiniwa katika viwango mbalimbali vya elimu, kwa mfano, Chuo Kikuu Makerere kina Idara ya Kiswahili ambayo hufundisha isimu na fasihi kwa Kiswahili. Pia, Chuo Kikuu cha Kyambogo, Chuo Kikuu cha Kampala na Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Mbale vinafundisha Kiswahili. Kiswahili ndiyo lugha ya mawasiliano ikitumiwa zaidi na askari.

Kwa upande wa Burundi, Kiswahili kinatumika sana Mashariki mwa Burundi. Kiswahili kinafundishwa katika baadhi ya vyuo, kwa mfano, Chuo cha Wanajeshi wa Bujumbura na katika Chuo Kikuu cha Bujumbura. Vilevile, Kiswahili hutumika katika Redio ya Taifa, Redio Buntu, Redio Rema, Redio Izere, Redio Bonesha, Redio Ibyizigiro, Redio Isanganiro na katika Televisheni ya Taifa ya Burundi. Baadhi ya vipindi vya redio na televisheni hizo ni kama vile habari, matangazo, vipindi vya utamaduni na mafunzo na matangazo ya mipira.

Nchini Rwanda, Kiswahili kinatumika sokoni na mijini. Aidha, kinafundishwa katika Chuo Kikuu cha Rwanda. Wapo baadhi ya wananchi wanaojiandikisha kujifunza Kiswahili katika madarasa ya jioni. Vilevile, Rwanda imeanzisha Kiswahili katika mtaala wa taifa na kuongezwa katika orodha ya lugha rasmi. Redio Rwanda kuanzia mwaka 1961 imekuwa na programu za Kiswahili kama vile taarifa ya habari, matangazo ya mpira na salamu za wasikilizaji. Hivi karibuni, lugha ya Kiswahili imeanza kufundishwa katika shule zote za upili nchini Rwanda. Pia, Serikali ya Rwanda imepanga kukifanya Kiswahili kuwa moja ya lugha za taifa za nchi hiyo.

Sudani Kusini lugha rasmi ni Kiingereza, pamoja na kutambulika kwa lugha mbalimbali za mitaa katika majimbo au miji, Kiswahili kinapangiwa kuenezwa nchini hasa baada ya Sudani Kusini kujiunga na Afrika Mashariki.

Kwa upande wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Kifaransa ni lugha rasmi. Kwa ujumla kuna lugha 242 hasa za Kibantu zinazozungumzwa Kongo. Kati yake lugha nne (4) zinatambulika kama lugha za kitaifa nazo ni Kikongo, Kingala, Kiluba na Kiswahili. Wakati wa ukoloni lugha hizo nne za kitaifa ziliwahi kutumiwa katika shule za msingi. Tangu mapinduzi ya 1997 sehemu za jeshi, hasa mashariki hutumia pia Kiswahili. Takriban 47% wanatumia Kifaransa kama lugha ya kwanza au lugha ya pili. (https://nasseryouth movement.net/sw/Kiswahili-Uchumi-Afrika-Mashariki-BAKITA).

Kwa upande wa mikakati yake ya maendeleo na kukuza utangamano ndani ya Jumuiya, JAM ilianzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) mwaka 2016 ili kuratibu maendeleo ya lugha hii. Kamisheni hutayarisha miongozo ya matumizi ya Kiswahili katika taasisi za jumuiya, kuendeleza istilahi na kusimamia tafsiri za kisheria na kiutawala (EAKC, 2019).

Nchi wanachama kama Tanzania, Kenya, Uganda Rwanda zimepitisha sera zinazokuza Kiswahili katika ngazi ya taifa au mawasiliano ya kitaifa. Mashirika ya kimataifa na taasisi za kitaaluma pia zimeunga mkono juhudi hizi kupitia mafunzo na makongamano. Mathalan, Dira ya Taifa ya mwaka 2050 inaeleza kuwa Kiswahili ndio lugha ya diplomasia. Ndio lugha ya kiuchumi ambayo itasaidia kutuunganisha katika miungano yetu ya kikanda (Dira ya Taifa, 2025). Katika sekta ya elimu, nchi nyingi za JAM zimeingiza Kiswahili katika mitaala ya shule na vyuo. Kenya imeifanya kuwa somo la lazima katika elimu ya msingi na sekondari. Uganda, Rwanda na Burundi zimepanua mafunzo ya walimu wa Kiswahili (Rugemalira, 2010). Aidha, tafsiri za nyaraka za JAM kutoka Kiingereza hadi Kiswahili zimeongezeka, jambo linaloimarisha usawa wa lugha na upatikanaji wa taarifa. Kwa ujumla, hatua hizi zinaweka msingi wa kukifanya Kiswazinaweka msingi wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya umma, ushirikianoshwaji na maendeleo leo ya kikanda.

## 2.0. Mkabala wa Kinadharia

Uchambuzi wa makala hii umejikita katika Nadharia ya Uchanganuzi Tunduizi Kilongo (NUTK) kwa kuzingatia michango ya Norman Fairclough na Teun van Dijk. Kwa mujibu wa - nadharia hii, lugha si chombo cha mawasiliano pekee, bali ni nyenzo inayobeba nguvu, utambulisho na uhusiano wa mamlaka katika jamii. Katika muktadha wa JAM, UTK hutumika kufakufafanua namna Kiswahili kinavyotumiwa kaka sanaa, michezo na utamaduni kama chombo cha kuimarisha mshikamano na utambulisho wa kikanda. Uchambuzi unazingatia maudhui ya kikijamii, kisiasa na kitamaduni yanayojitokeza katika matamasha, mashindano ya michezo na maonesho ya tamaduni ndani ya JAM.

Aidha, makala imeungwa mkono na Nadharia ya Itikadi za Lugha kama ilivyoelezwa na Kathryn Woolard na Michael Silverstein. Nadharia hii huchunguza mitazamo ya jamii kuhusu thamani, uhalali na nafasi ya lugha fulani. Nchi nynyingi wanachama wa JAM hukitambua Kiswahili kama lugha ya taifa au ya maendeleo na kuakisi itikadi zao kuhusu umoja na maendeleo ya kijamii. Kwa kuunganisha UTK UTK na Itikadi za Lugha, makala inachambua matumizi ya Kiswahili pamoja na maana zake za kijamii na kisiasa katika sanaa, michezo na utamaduni wa kikanda.

## 3.0. Mbinu ya Uchunguzi

Uchunguzi huu ulilenga kuchambua matumizi na uthamini wa Kiswahili katika sanaa, michezo na utamaduni ndani ya nchi wanachama wa JAM. Utafiti ulitumia mkabala wa mbinu mchanganyiko uliounganisha ukusanyaji na uchambuzi wa data za kimaelezo. Mkabala huu uliwezesha kupatikana kwa taarifa za kina kuhusu hali halisi ya matumizi ya Kiswahili pamoja na mitazamo ya wadau kuhusu nafasi, changamoto na fursa zake. Data zilikusanywa kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda. Nchi hizi ziliteuliwa kwa kuzingatia ushiriki wao katika sera na programu za kukuza Kiswahili ndani ya JAM. Ukusanyaji wa data ulifanyika kati ya Julai na Septemba 2024.

Sampuli ilihusisha watoataarifa 30, sita kutoka kila nchi. Usampulishaji lengwa ulitumika ili kupata washiriki wenye uelewa na uzoefu wa moja kwa moja katika matumizi ya Kiswahili kwenye sekta husika. Kila kundi la nchi lilijumuisha mhadhiri wa Kiswahili, mwandishi wa habari, msanii, mwanamichezo, mratibu wa shughuli za utamaduni na mfasiri au mtaalamu wa lugha. Uteuzi ulizingatia uzoefu wa kitaaluma na mchango wao katika kukuza au kutumia Kiswahili katika mazingira ya kazi na jamii. Data za msingi zilikusanywa kwa mbinu ya usaili wa mtandaoni na hojaji za kidijiti. Usaili ulitumika kupata maelezo ya kina kutoka kwa wahadhiri, waandishi wa habari na wasanii, huku hojaji zikitumika kwa wanamichezo na waratibu wa utamaduni kwa ufanisi wa muda. Maswali yalihusu matumizi ya Kiswahili, changamoto na mapendekezo ya uboreshaji.

## 4.0. Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Sehemu hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka kwa watoataarifa walioshiriki katika utoaji wa taarifa za utafiti huu.

### 4.1. Kiswahili na Sanaa katika JAM

Katika sehemu hii, mwandishi anafafanua kuhusu nafasi ya Kiswahili na sanaa katika nchi za JAM. Uchunguzi huu umebaini kuwa Kiswahili kinapewa hadhi kama lugha ya ubunifu wa fasihi, lugha ya ushirikiano wa wasanii na lugha ya kutumiwa katika vyombo vya habari za michezo.

#### 4.1.1. Kiswahili kama Lugha ya Ubunifu wa Fasihi na Sanaa za Maonesho

Kiswahili ni mhimili wa ubunifu wa fasihi na sanaa za maonesho Afrika Mashariki, kikitumika kuwasilisha hisia, historia na maadili kupitia muziki, ushairi na maigizo (EAKC, 2019). Uchunguzi umeonesha kuwa wasanii wengi hukitumia Kiswahili kama lugha kuu kwa sababu za utambulisho, upana wa hadhira na mshikamano wa kijamii. Mwandishi kutoka Tanzania alieleza:

“Kiswahili hunipa nafasi ya kugusa nyanja nyingi za kijamii kupitia kazi bunifu. Kwa mfano, kupitia tamthilia zangu, ninapata kuzungumzia masuala ya siasa, uchumi na utamaduni. Lugha hii ni pana kwa sababu inatumiwa na watu wengi” (Mtoataarifa Na. 3, Tanzania, 2024).

Kauli hii inaangazia nafasi ya Kiswahili kama chombo cha ujenzi wa mawazo na ubunifu, jambo linalohusiana na NUKT (Fairclough, 1995), ambayo huona lugha kama njia ya kuunda maana katika mazingira ya kijamii. Hivyo, wasanii hushughulikia masuala ya kijamii yanayohusu watu wengi wa ukanda wa JAM kwa kutumia Kiswahili. Hali ambayo hujenga mshikamano wa kijamii na utambulisho wa pamoja katika ukanda huu. Hoja hii inaonesha kuwa Kiswahili si tu lugha ya sanaa, bali pia lugha ya mawasiliano yenye nguvu za mabadiliko ya kijamii.

#### 4.1.2. Ushirikiano wa Wasanii wa JAM Kupitia Kiswahili

Kiswahili kimekuwa nguzo muhimu inayowezesha ushirikiano wa kisanii kati ya wasanii kutoka nchi mbalimbali za JAM kupitia matamasha, maonesho ya sanaa na mashindano ya kikanda. Data kutoka kwa watoataarifa inaonesha kuwa lugha hii hutumiwa kama jukwaa la kuwasiliana, kujifunza na kushirikiana baina ya wasanii, hivyo kupunguza vikwazo vya lugha vya kitaifa. Msanii mmoja kutoka Uganda alisema:

“Nilipoanza kushirikiana na wasanii kutoka Kenya na Tanzania, tuliamua kutumia Kiswahili kama lugha ya kazi yetu ya sanaa za mitaani, ikatusaidia kuelewana kirahisi na kuwasilisha ujumbe wetu kwa hadhira pana”. (Mtoataarifa Na. 11, Uganda, 2024).

Kauli hiyo inaonesha ushirikiano wa wasanii wa JAM kupitia sanaa. Hali hii inaakisi mtazamo wa Woolard (1998:3), ambao unaeleza kwamba matumizi ya lugha fulani hujengwa kwa- imani za kijamii kuhusu thamani yake. Katika muktadha huu, wasanii huona Kiswahili si tu kama chombo cha mawasiliano, bali pia kama chombo cha ujumuishi na fursa ya kiuchumi. Zaidi, tamasha kama Jukwaa la Sanaa Afrika Mashariki na ‘Swahili International Expo’ yamechangia kuhimiza maonesho ya Kiswahili kwa wasanii wa ukanda huu. Hii inaonesha kuwa Kiswahili ni nyenzo ya kuvuka mipaka ya kitaifa na kukuza sanaa inayozungumza lugha moja ya utambulisho wa Kiafrika.

#### 4.1.3. Matumizi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari vya Kisanaa

Kiswahili kimepata nafasi pana katika vyombo vya habari vya sanaa kama runinga, redio na majukwaa ya mtandaoni kama YouTube, ambapo vipindi vya sanaa huchochea mijadala, burudani na elimu katika jamii. Kwa mujibu wa watoa taarifa, vipindi vya redio na televisheni kama Wasafi TV, KBC Swahili Drama, Bongo la Biashara na Blogu za sanaa za YouTube zimekuwa maarufu katika nchi wanachama kwa kutumia Kiswahili kwa ufasaha. Mfasiri kutoka Kenya alibainisha:

“Vipindi vya sanaa vinavyotumia Kiswahili vinawafikia watu wengi, hata wale wasio na elimu ya juu. Hii imepanua wigo wa mashabiki na wachangiaji wa sanaa”. (Mtoataarifa Na. 17, Kenya, 2024).

Kwa mujibu wa UTK, vyombo vya habari havitoi habari pekee, bali ni majukwaa ya kutengeneza uhalisia wa kijamii. Hivyo basi, matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari vinavyohusiana na sanaa huendeleza itikadi ya umoja wa kitamaduni, huku vikichochea mazungumzo ya umma kuhusu sanaa kama sehemu ya maisha ya kila siku. Kwa njia hii, Kiswahili kinapandisha hadhi ya sanaa kwa kuiwasilisha katika lugha inayoeleweka, inayopendwa na inayomilikiwa na watu wa Afrika Mashariki.

## 4.2. Kiswahili katika Michezo

Sehemu hii inachambua nafasi ya Kiswahili katika nchi za JAM kupitia michezo. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa Kiswahili kinatumika katika matamasha ya michezo, mshikamano wa mashabiki na wanamichezo.

### 4.2.1. Kuwapo kwa Kiswahili katika Matamasha ya Michezo ya JAM

Kiswahili ni lugha kuu ya mawasiliano katika matamasha ya michezo ya JAM, yakiwamo Michezo ya Shule za Sekondari, Mashindano ya Mabunge na Mashindano ya Vyuo Vikuu. Hutumika katika hotuba za ufunguzi, matangazo rasmi, mabango ya kuhamasisha na mawasiliano ya moja kwa moja kati ya wachezaji na waandaaji. Mwanamichezo kutoka Rwanda alieleza:

"Wakati wa mashindano ya shule za Afrika Mashariki tulitumia Kiswahili kuwasiliana na waamuzi na hata wapinzani wetu, jambo lililorahisisha ushirikiano bila tafsiri". (Mtoataarifa Na. 24, Rwanda, 2024).

Ushahidi huo unaonesha kuwa Kiswahili hutumika kama daraja la mawasiliano katika mazingira ya kimichezo ambapo washiriki hutoka katika mataifa yenye lugha tofauti. Kwa mujibu wa NUTK (Fairclough, 1995), lugha hutumika kujenga mazingira na kuimarisha uhusiano wa kijamii. Matumizi ya Kiswahili katika michezo huonesha kuwa lugha hii si chombo cha mawasiliano pia ni msingi wa kujenga mshikamano wa kikanda kupitia michezo. Hali hii hutoa fursa ya kuunganisha vijana na watu wa mataifa tofauti kwa lugha moja inayomilikiwa na watu wengi.

### 4.2.2. Kiswahili kama Lugha ya Mshikamano wa Wachezaji na Mashabiki

Katika muktadha wa michezo, Kiswahili hujenga mshikamano wa kijamii kati ya wachezaji, mashabiki na wadau wa michezo kwa sababu ya uwezo wake wa kueleweka kirahisi na kupokelewa kiutamaduni. Mashabiki huimba nyimbo za hamasa, kushiriki midahalo mitandaoni na kutoa maoni kupitia redio na runinga kwa kutumia Kiswahili. Kocha kutoka Kenya alibainisha:

"Tuliona timu yetu ikipokelewa vizuri tulipowasili Uganda kwa sababu tulizungumza Kiswahili. Mashabiki walitukaribisha kama ndugu. Kiswahili kilivunja ukuta wa tofauti za kitaifa". (Mtoataarifa Na. 10, Kenya, 2024).

Kauli hiyo inaakisi mitazamo chanya ya lugha kama sehemu ya utambulisho wa pamoja, ikihusishwa na Nadharia ya Itikadi za Lugha (Woolard, 1998), ambayo huonesha kuwa lugha hujengwa katika misingi ya kijamii, kiutamaduni na kihisia. Katika michezo, hisia na mshikamano vina nafasi kubwa, hivyo Kiswahili hutoa jukwaa la kuunganisha watu kupitia hamasa ya pamoja. Hii inathibitisha kuwa lugha hii si chombo cha taarifa pekee, vilevile ni njia ya kujenga utangamano wa jamii na kukuza mshikamano wa kikanda kupitia uzoefu wa michezo.

### 4.2.3. Nafasi ya Kiswahili katika Nyimbo, Kaulimbiu na Uandishi wa Habari za Michezo

Kaulimbiu na Uandishi wa Habari za Michezo
Kiswahili kimepewa nafasi muhimu katika utunzi wa nyimbo za michezo, kaulimbiu za mashindano na uandishi wa habari unaohusu michezo katika vyombo mbalimbali vya habari. Nyimbo kama "Tuko Pamoja", "Vijana wa EAC" na kaulimbiu kama "Umoja kupitia Michezo" zikihamasisha mshikamano na uzalendo wa Kiafrika. Mwanahabari kutoka Burundi alisema:

"Tunatumia lugha ya Kiswahili kuandika makala za michezo kwa sababu huwaunganisha wasomaji wengi wa Afrika Mashariki. Lugha hii hufikisha ujumbe kwa wepesi na kwa hisia". (Mtoataarifa Na. 15, Burundi, 2024).

Kwa mujibu wa van Dijk (2001:32) katika muktadha wa UTK, lugha katika vyombo vya habari hutengeneza mitazamo ya kijamii na kuimarisha majukwaa ya majadiliano ya umma. Hivyo, Kiswahili katika habari za michezo sio tu lugha ya taarifa,

pia ni njia ya kushirikisha umma katika matukio ya pamoja, kuhamasisha ushiriki wa kijamii na kujenga lugha ya pamoja ya michezo. Kaulimbiu na nyimbo zinazotumia Kiswahili huimarisha hali ya kiushindani kwa heshima, changamot, utambulisho, na hisia ya kuwa sehemu ya familia ya JAM.

### 4.3. Kiswahili na Utamaduni wa JAM

Sehemu hii inafafanua nafasi ya Kiswahili katika nchi za JAM kupitia utamaduni. Nafasi hiyo imeangaziwa katika ngoma, mila, mavazi na mapishi ya jadi, urithi na maonesho ya utamaduni.

#### 4.3.1. Matumizi ya Kiswahili katika Ngoma, Mila, Mavazi na Mapishi ya Jadi

Kiswahili kinajitokeza kama lugha inayoratibu na kuwasilisha vipengele muhimu vya utamaduni wa jamii za JAM, ikiwa ni pamoja na ngoma, mila, mavazi na mapishi ya jadi. Katika maonesho ya ngoma za asili, wasanii huanza na salamu, maelezo au shairi fupi kwa Kiswahili kabla ya maonesho, wakieleza maana ya ngoma husika na ujumbe wake wa kiutamaduni. Mtoataarifa mmoja kutoka Tanzania alibainisha:

"Tunapocheza ngoma kama Chakacha au Mdundiko kwenye matamasha ya kikanda, tunatumia Kiswahili kueleza historia na dhamira ya ngoma hizo kwa hadhira mbalimbali". (Mtoataarifa Na. 2, Tanzania, 2024).

Kauli hiyo inaonesha kuwa Kiswahili hufanya kazi kama lugha ya kufasiri urithi wa kitamaduni ili uweze kueleweka kwa jamii pana ya JAM. Kwa mujibu wa UTK, lugha hufanikisha uundaji na uwasilishaji wa maudhui ya kijamii. Kiswahili, kwa muktadha huu, husaidia kusambaza maana za kitamaduni kutoka jamii moja hadi nyingine, hivyo kuimarisha uelewano wa tamaduni ndani ya Jumuiya. Kwa njia hii, lugha inakuwa sio tu kuwa ni chombo cha mawasiliano bali mhimili wa kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa eneo hili.

#### 4.3.2. Kiswahili kama Lugha ya Turathi

Kiswahili kinatambuliwa kama lugha ya urithi wa pamoja katika nchi za JAM, kwa sababu kimekua, kimepanuka na kimeboreshwa katika jamii nyingi za ukanda huu. Lugha ya Kiswahili imekuwa nyenzo muhimu katika kuibua fursa nyingi ambazo zinaweza kutumika kukuza diplomasia ya uchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Data za uchunguzi zinaonesha kuwa Kiswahili kinaeleweka na kutumiwa kwa kiwango kikubwa katika shughuli za kijamii na jamii nyingi zinajivunia kuwa sehemu ya historia ya lugha hii. Mtaalamu wa lugha kutoka Rwanda alisema:

"Ingawa Kiswahili si lugha mama kwa wengi nchini kwetu, sasa kinaonekana kama lugha ya utambulisho wa Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, ni yetu sote". (Mtoataarifa Na. 26, Rwanda, 2024).

Kauli hii inaakisi maono ya Nadharia ya Itikadi za Lugha (Woolard, 1998), ambayo inaeleza kuwa mitazamo ya kijamii kuhusu lugha huathiri matumizi na nafasi ya lugha hiyo. Mataifa ya JAM yanaendelea kukuza fikra kwamba Kiswahili ni urithi wa pamoja unaoweza kuimarisha mshikamano wa kikanda. Kwa msingi huo, Kiswahili kinajenga msingi wa urithi wa pamoja wa kitamaduni unaoambatana na historia, mawasiliano na maadili ya jamii mbalimbali, hivyo kuimarisha maono ya Umoja wa Kiafrika ndani ya Jumuiya.

#### 4.3.3. Nafasi ya Kiswahili katika Maonesho ya Utamaduni

Katika maonesho ya utamaduni kama Tamasha la Utamaduni, Jukwaa la Utamaduni wa Kiswahili na Makongamano ya Kiswahili, Kiswahili hutumika kama lugha rasmi ya utambulisho, maelezo ya maonesho, matangazo na mijadala.Mchanganyiko wa mataifa mbalimbali katika matukio haya hufanikishwa na matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kati. Mtoataarifa kutoka Kenya alisema:

"Tuliposhiriki katika maonesho ya mavazi ya kitamaduni Zanzibar, tulibidi kujifunza Kiswahili kidogo ili kueleza kazi zetu na ikatusaidia kuvutia watu wengi zaidi". (Mtoataarifa Na. 6, Kenya, 2024).

Kwa mujibu wa van Dijk (2001) katika muktadha wa UTK, lugha ni chombo cha kushiriki mamlaka ya kijamii na kuonesha nafasi ya mtu au kikundi katika jamii.

Maonesho haya yanapowasilishwa kwa Kiswa -hili, yanawapa washiriki wa JAM jukwaa la kujieleza kwa usawa, bila kizuizi cha lugha za za kikoloni.

Hili huongeza ujumuishaji wa jamii katika mazungumzo ya kitamaduni na huongeza thamani ya Kiswahili kama lugha ya ubunifu, mawasiliano na biashara. Kwa msingi huu, Kiswahili hubeba dhamana ya kitamaduni na kiuchumi katika matukio ya kikanda, yakihimiza uelewano na mshikamano miongoni mwa mataifa wanachama.

## 4.4 Ulinganisho wa Matumizi ya Kiswahili katika Sanaa, Michezo na Utamaduni

Uchunguzi wa makala hii umebaini kuwa kuna tofauti ya matumizi katika sekta za sanaa, michezo na utamaduni kwa nchi za JAM kama tunavyoona katika jedwali lifuatalo linaonesha:

**Jedwali la 2: Ulinganisho wa Matumizi ya Kiswahili katika Sanaa, Michezo na Utamaduni**

| Nchi | Sanaa | Michezo | Utamaduni |
|---|---|---|---|
| Tanzania | 5 | 4 | 5 |
| Kenya | 4 | 4 | 4 |
| Uganda | 3 | 3 | 3 |
| Burundi | 2 | 2 | 2 |
| Rwanda | 2 | 2 | 3 |

**Chanzo:** Uchunguzi wa Makala, 2024

Katika jedwali hapo juu tunaona kuwa Tanzania inaongoza kwa matumizi ya Kiswahili katika sekta zote, ikifuatiwa na Kenya. Uganda ina kiwango cha wastani, huku Burundi na Rwanda zikiwa na matumizi duni, kunakoashiria tofauti za kisera na kijamii kuhusu nafasi ya Kiswahili.




**Chanzo:** Uchunguzi wa Makala, 2024

Grafu inaonesha ulinganisho wa kiwango cha matumizi ya Kiswahili katika sanaa, michezo na utamaduni kwa nchi tano wanachama wa JAM kwa kipimo cha 1 hadi 5. Tanzania inaongoza katika sekta zote tatu. Imepata alama 5 katika sanaa na utamaduni na alama 4 katika michezo. Hii inaonesha kuwa Kiswahili kimejengeka kama mhimili wa utambulisho wa taifa na kimetumika kwa kiwango kikubwa katika maonesho ya kisanaa, urithi wa kitamaduni na mashindano ya michezo. Kenya inafuata kwa karibu ikiwa na alama 4 katika sekta zote. Matokeo haya yanaashiria matumizi makubwa ya Kiswahili katika burudani, vyombo vya habari na midahalo ya michezo, ingawa nafasi yake huathiriwa na hadhi pana ya Kiingereza katika maeneo rasmi.

Uganda inaonesha matumizi ya wastani kwa kupata alama 3 katika sekta zote. Kiswahili kinaanza kupanuka katika vyombo vya habari na michezo, lakini bado hakijaimarishwa kikamilifu katika sera za elimu na utamaduni. Burundi imepata alama 2, jambo linaloashiria matumizi duni. Ingawa lugha hutumika katika biashara na mawasiliano ya kijamii, haijapata nafasi thabiti katika sanaa na michezo. Rwanda pia ina alama 2 katika sanaa na michezo, lakini imepata alama 3 katika utamaduni. Hali hii inaonesha juhudi za hivi karibuni za kuimarisha Kiswahili kupitia sera za lugha na mabadiliko ya mitaala.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha tofauti za maendeleo ya Kiswahili katika nchi wanachama. Zinathibitisha kuwa pale lugha inapopewa kipaumbele cha kisera na kijamii, huimarika katika sekta za ubunifu na utamaduni. Hivyo, kuna haja ya mkakati wa pamoja wa kikanda ili kupunguza pengo la matumizi na kukuza mshikamano kupitia Kiswahili.

## 5.0. Changamoto na Fursa

Katika sehemu hii, mtafiti anabainisha changamoto na fursa zinazopatikana kutokana na matumizi ya Kiswahili katika nchi za JAM:

### 5.1. Changamoto

Matokeo ya uchunguzi wa makala hii yana-onesha kuwa kuna changamoto mbalimbali zinazohusu matumizi ya Kiswahili katika nchi za JAM, kama ifuatavyo:

#### 5.1.1. Ukosefu wa Mwongozo wa Pamoja wa Sera za Lugha katika JAM

Moja ya changamoto kubwa inayokwamisha matumizi ya Kiswahili katika sanaa, michezo na utamaduni ni ukosefu wa sera thabiti na zenye mlingano miongoni mwa nchi wanachama wa JAM. Ingawa baadhi ya mataifa kama Tanzania na Kenya zimeweka Kiswahili kama lugha ya taifa na kufundishwa shuleni, mataifa mengine bado yanakikumbatia Kiingereza au Kifaransa kama lugha kuu ya utendaji. Mtoa taarifa kutoka Burundi alisema:

"Hapa kwetu Kiswahili hakifundishwi kama somo la lazima; wengi hukijua kwa sababu ya biashara au muziki tu". (Mtoataarifa Na. 28, Burundi, 2024).

Hali hii huonesha pengo kubwa la kisera kati ya nchi, linalopunguza juhudi za pamoja za kuimarisha Kiswahili. Kwa mujibu wa Nadharia ya Itikadi za Lugha (Woolard, 1998), mitazamo ya mamlaka kuhusu lugha huathiri moja kwa moja matumizi yake kijamii. Bila sera za pamoja za lugha, juhudi za kuunganisha jamii za JAM kupitia Kiswahili hukwama. Hili linaashiria haja ya kuwapo kwa mkataba wa kikanda wa lugha ambao utaimarisha nafasi ya Kiswahili katika nyanja za kijamii na kitamaduni kwa mataifa yote.

#### 5.1.2. Mitazamo Hasi kuhusu Kiswahili kama Lugha ya Sanaa na Maarifa ya Kisasa

Katika baadhi ya nchi za JAM, Kiswahili bado kinatazamwa kuwa lugha ya kila siku inayofaa tu kwa mawasiliano ya kawaida na si kama lugha ya sanaa ya juu au maarifa ya kitaaluma. Mtoataarifa Na. 13 kutoka Uganda alieleza:

"Wengi bado wanaamini kwamba kazi za sanaa zilizoandikwa au kuoneshwa kwa Kiingereza ni za kisasa na zenye hadhi zaidi kuliko zile za Kiswahili". (Mtoataarifa Na. 13, Uganda, 2024).

Mitazamo kama hii huathiri wasanii chipukizi, ambao huchagua lugha nyingine kwa matarajio ya soko pana au heshima ya kazi zao. Hali hii inathibitisha maelezo ya UTK (Fairclough, 1995), kwamba lugha huathiriwa na mitazamo ya kijamii na hujengwa katika miundo ya nguvu na mamlaka. Wakati Kiswahili kinapodunishwa au kuonekana cha chini kihadhi, hadhira yake hupungua na wasanii hukosa motisha ya kukitumia. Kwa hiyo, mabadiliko ya mitazamo kuhusu thamani ya Kiswahili ni muhimu ili kukifanya kuwa lugha ya heshima na ubunifu wa kisasa.

#### 5.1.3. Changamoto za Mfumo wa Elimu na Ukosefu wa Wataalamu wa Kiswahili

Mfumo wa elimu katika nchi nyingi wanachama wa JAM haujakipa Kiswahili nafasi ya msingi na muhimu kama lugha ya taaluma au ubunifu wa kisanaa.
Hali hii pia, inachangiwa na ukosefu wa walimu wa Kiswahili waliohitimu, vitabu vya kufundishia na miundombinu ya kukuza lugha katika taasisi za elimu. Mhadhiri kutoka Rwanda alieleza:

"Hata vyuo vikuu vina upungufu wa wahadhiri wa Kiswahili, jambo linalorudisha nyuma maendeleo ya lugha hii katika muktadha wa kitaaluma na utamaduni". (Mtoataarifa Na. 22, Rwanda, 2024).

Kwa mujibu wa van Dijk (2001), lugha huimarishwa kwa kupewa nafasi katika taasisi rasmi kama shule na vyuo, ambako uamuzi wa kisera hutekelezwa. Kwa hiyo, kukosekana kwa miundo madhubuti ya kitaaluma ya kukuza Kiswahili kunapunguza ufanisi wake katika kuendeleza sanaa na utamaduni. Hii inahitaji juhudi za kuongeza wataalamu wa Kiswahili na kuweka sera thabiti za lugha katika elimu ya juu.

### 5.2. Fursa

Matokeo ya uchunguzi wa makala hii yana-onesha kuwa kuna fursa mbalimbali zinazopatikana zinazotokana na matumizi ya Kiswahili katika nchi za JAM:

### 5.2.1. Fursa Zilizopo kupitia Taasisi za Kukuza Kiswahili

Pamoja na changamoto zilizopo, fursa za kukuza nafasi ya Kiswahili katika sanaa, michezo na utamaduni ni pana, hasa kupitia taasisi za kitaifa na kikanda. Taasisi kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Baraza la Kiswahili la Taifa, Chama cha Kiswahili cha Taifa na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki zimechangia usanifishaji wa istilahi, mafunzo ya wataalamu, ubadilishanaji wa wataalamu na uhamasishaji wa matumizi rasmi ya lugha. Mtoataarifa Na. 4 kutoka Kenya alisimulia:

"Tumeanza kuona mabadiliko chanya kupitia juhudi za BAKITA na Kamisheni ya EAC, hasa kwenye tafsiri za nyaraka na programu za redio za Kiswahili". (Mtoataarifa Na. 7, Kenya, 2024).

Hii inaonesha kuwa taasisi hizi ni injini ya kuendeleza Kiswahili na zinaweza kuwa nguzo kuu ya mageuzi ya lugha. Kwa mujibu wa Fairclough (1995) taasisi ni sehemu ya miundo ya kijamii inayoweza kubadilisha mitazamo na nafasi ya lugha. Hivyo, kuimarisha ushirikiano kati ya wadau hawa na serikali za kitaifa ni njia bora ya kuimarisha Kiswahili katika nyanja za kijamii.

### 5.2.2. Uhamasishaji wa Kidijiti na Teknolojia kama Fursa ya Kukuza Kiswahili

Teknolojia ya habari na mawasiliano imeibuka kuwa jukwaa lenye fursa kubwa kwa ukuzaji wa Kiswahili, hasa kupitia majukwaa ya mitandao ya kijamii, *YouTube*, redio za mtandaoni na maonesho ya sanaapepe. Wasanii wengi wa JAM sasa hutumia Kiswahili kwenye maudhui ya kidijiti ili kuvutia watazamaji kutoka maeneo mbalimbali ya ukanda huu. Msanii kutoka Tanzania alifafanua:

"Kupitia *TikTok na YouTube,* nimeweza kuwafikia mashabiki Kenya, Uganda na hata Burundi na wote tunawasiliana kwa Kiswahili". (Mtoataarifa Na. 5, Tanzania, 2024).

Hali hii inaonesha kuwa Kiswahili kina uwezo mkubwa wa kuvuka mipaka ya kitaifa kupitia teknolojia. Kwa mujibu wa Woolard (1998), watu huchagua lugha kutokana na muktadha wa kijamii na fursa zinazotokana nayo. Teknolojia inapotumiwa vyema, Kiswahili huonekana kuwa lugha ya kisasa, ubunifu na fursa za kiuchumi. Kwa hivyo, kuwekeza katika maudhui ya kidijiti kwa Kiswahili ni mkakati unaoweza kubadilisha mtazamo wa lugha hii na kuimarisha nafasi yake katika jamii.

### 5.3. Mapendekezo ya Kuimarisha Nafasi ya Kiswahili katika JAM

Ili kuhakikisha Kiswahili kinachukua nafasi yake ipasavyo katika sanaa, michezo na utamaduni wa JAM, hatua madhubuti na za pamoja zinapaswa kuchukuliwa na wadau wa kitaifa na kikanda, kama ifuatavyo:

Kwanza, ni muhimu kwa kila nchi mwanachama wa JAM kupitisha sera thabiti na zenye ufanisi zinazotambua Kiswahili kama lugha ya maendeleo, utambulisho na urithi wa pamoja. Hii inapaswa kuambatana na utekelezaji wa sera hizo kwa vitendo katika taasisi za elimu, utawala na burudani.

Pili, kuna haja ya kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili katika ngazi zote za elimu kwa kuongeza idadi ya walimu waliobobea, kuandaa vifaa vya kujifunzia vya kisasa na kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakuwa somo la lazima angalau katika elimu ya msingi na sekondari katika nchi zote za JAM.

Tatu, taasisi za kukuza Kiswahili kama TATAKI, BAKITA, KAKAMA, CHAKITA, CHAKAMA na nyinginezo zishirikiane kwa karibu na mashirika ya sanaa, vyama vya michezo na vituo vya utamaduni ili kupanua matumizi ya Kiswahili hadi katika jamii za pembezoni na mikoani. Ushirikiano huu unaweza kuleta athari kubwa kupitia matamasha ya utamaduni, mashindano ya kisanaa na programu za kukuza vipaji vinavyotumia Kiswahili.

Nne, serikali za JAM zipewe msukumo wa kuanzisha au kuongeza ruzuku, mafunzo na majukwaa ya kidijiti kwa wasanii, wanamichezo na vikundi vya tamaduni vinavyotumia Kiswahili, ili kuongeza uzalishaji na usambazaji wa maudhui ya Kiswahili yanayovutia na kuelimisha.

Tano, vyombo vya habari vya kitaifa na vya kikanda visisitize matumizi ya Kiswahili katika vipindi vya michezo, sanaa na utamaduni kwa kutoa muda maalum wa kurusha maudhui hayo, pamoja na kuanzisha tuzo na mashindano ya vipindi bora vya Kiswahili. Hii itahamasisha ubunifu wa kisanaa unaotumia Kiswahili na kuvutia hadhira kubwa zaidi.

## 6.0 Hitimisho

Kwa kuzingatia uchambuzi wa makala hii, imebainika kuwa Kiswahili kina nafasi ya kimkakati katika kukuza sanaa, michezo na utamaduni ndani ya nchi wanachama wa JAM. Matokeo yanaonesha kuwa lugha hii inatumika kwa mapana katika fasihi, muziki, maigizo na vipindi vya utamaduni. Vilevile, imeimarisha mshikamano wa kijamii kupitia mashindano ya michezo na matamasha ya sanaa ya kikanda. Kiswahili kimeendelea kuwa jukwaa la kuwasilisha urithi wa kitamaduni, kujenga utambulisho wa pamoja na kuchochea ubunifu wa kisasa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Hata hivyo, changamoto bado zipo. Mitazamo hasi kuhusu hadhi ya Kiswahili, udhaifu wa utekelezaji wa sera za lugha na uhaba wa wataalamu vinaathiri upanuzi wa matumizi yake. Katika muktadha wa kijamii na kisiasa wa JAM, Kiswahili kina thamani kama chombo cha utambulisho wa Kiafrika na mshikamano wa kikanda. Si lugha ya mawasiliano tu, bali pia ni nyenzo ya kubeba maarifa, mila na matarajio ya jamii za Afrika Mashariki. Kwa msingi huo, makala inapendekeza kuongezwa kwa uwekezaji katika elimu ya Kiswahili, uimarishaji wa sera,maendeleo ya istilahi na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano. Serikali, taasisi za lugha, wasanii na wanamichezo wanapaswa kushirikiana katika kuendeleza sekta za ubunifu kwa kutumia Kiswahili. Hatua hizi zitaimarisha utambulisho wa kikanda na kuchochea maendeleo jumuishi kupitia sanaa, michezo na utamaduni.

## MAREJELEO


Batibo, H. M. (2005). Language Decline and Death in Africa: Causes, Consequences and Challenges. Multilingual Matters.

Blommaert, J. (2014). State Ideology and Language in Tanzania: Second and Revised Edition. Edinburgh University Press.

EAKC (2019). Capacity Assessment of the Development and Use of Kiswahili in the EAC. Arusha: EAC.

Fairclough, N. (1995). Critical Discourse Analy sis: The Critical Study of Language. Longman.

Karanja, L. W. (2003). Language in Education and Language Policy in East Africa. Oxford: African Books Collective.

Katoke, I. (2004). History of East Africa. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Kiango, J. G. (2015). Kiswahili katika Ukanda wa Afrika Mashariki: Mwelekeo wa Kijamii na Kiutamaduni. Nairobi: Longhorn Publishers.

Legère, K. (2006). Promoting the Use of African Languages in Education: A Case of Kiswahili. In: UNESCO Conference Papers on Multilingual ism.

Mazrui, A. M., & Mazrui, A. A. (1998). The Power of Babel: Language and Governance in the African Experience. University of Chicago Press.

Mulokozi, M. M. (1999). Kiswahili na Maende leo ya Afrika. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchun guzi wa Kiswahili (TUKI).

Ntabo, R. (2017). "Kiswahili katika Maendeleo ya Jamii ya Afrika Mashariki". Jarida la Kiswahili, 83(2), 45-61.

Rugemalira, J. M. (2010). "The Spread of Kiswahili in East Africa: A Historical Perspective". TUKI Journal of African Languages, Vol. 5.

Silverstein, M. (1979). "Language Structure and Linguistic Ideology". In The Elements: A Paras ession on Linguistic Units and Levels.

van Dijk, T. A. (2001). Discourse and Power. Palgrave Macmillan.

Woolard, K. (1998). "Language Ideology as a Field of Inquiry". Language Ideologies: Practice and Theory, 3-47.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2025), *Dira ya Taifa 2050*

(https://nasseryouthmovement.net/sw/Kiswahili-Uchumi-Afrika-Mashariki-BAKITA). Imesomwa tarehe 19, Mei, 2026.